الجامعة السعودية الالكترونية
Saudi Electronic University
2011 1432

Arabic-Online.net
العربية على الإنترنت

# Kiarabu Online

Mpango wa Kiarabu Mtandaoni ni mpango wa mtandaoni na njia mpya katika historia ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili. Mpango ni mfano mpya wa mafunzo unaotolewa na Chup kikuu cha Mtandaoni cha Saudia ili kufunza lugha ya Kiarabu. Ninaweza kuendelea kwa kupendekeza kwamba mpango wa kujifunza Kiarabu kama lugha ya kigeni unapatikana mahali popote, wakati wowote, duniani kote. Kwa sababu ya uzuri wa mpango wa aina hii, lugha ya Kiarabu inaweza kuchukuliwa duniani kote.

**Mkuu wa Chuo kikuu cha Mtandaoni cha Saudia**

**Dkt. Abdullah bin Abdulaziz Al Mosa**

Jua la Kiarabu linachomoza duniani



# Lugha ya Kiarabu

Lugha ni daraja kati ya tamaduni. Ni zaidi ya kuwa njia ya mawasiliano kati ya watu wa taifa; ni hifadhi kubwa ya utofauti wa kitamaduni na urejeshaji wa mahusiano, njia ya kufahamu tamaduni, na njia ya kukuza ushirikiano mpana kati ya mataifa.

Lugha ya Kiarabu imekuwa katika mstari wa mbele katika kuhifadhi utamaduni wa binadamu. Inazungumzwa sasa katika nchi 22 na watu milioni 422 na imeshawishi pakubwa ubinadamu. Ni lugha kuu inayotumiwa na zaidi ya Waisilamu bilioni moja na nusu duniani kote, na moja ya lugha sita za Umoja wa Mataifa, inasheherekewa na UNESCO kila mwaka.

Kumekuwa na hitaji linaloongezeka kutoka kwa wanenaji wengine wa lugha kujifunza Kiarabu kwa malengo tofauti. Sasa kuna hitaji la haraka, katika ulimwengu wa sasa, kwa mawasiliano ya kitamaduni na ustaarabu kati ya Waarabu na watu wengine duniani kote.

Kwa sasa, kuna ukosefu wa mpango tondoti na uliojumuishwa wa mpango wa mtandaoni katika nyanja ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili ambao unaweza kutoa mtalaa wa juu wa kielimu wenye mitihani iliyosawazishwa, il hali ikishughulikia ukosefu unaowezekana katika taasisi za kawaida za kujifunza lugha ya Kiarabu.

Licha ya hayo, kuna hitaji la haraka la kukuza vilivyo mafunzo ya Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili ili kukuza jukumu la Saudia katika kusambaza Kiarabu na utamaduni wa Kiislamu ambao unakuza ufahamu na kuishi pamoja kwa amani kati ya mataifa na tamaduni/

Kwa kuwa Wizara ya Elimu ya Saudia imekuwa makini katika kukuza lugha ya Kiarabu, Chup kikuu cha Mtandaoni cha Saudia kimechukua hatua muhimu ya kufikia mahitaji yaliyo hapa juu kwa kuchukua hatua kubwa katika nyanja ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili, kutumia njia na mpango mahiri kwa kutekeleza uvumbuzi wa Arabic-Online.net, uvumbuzi anzilishi wa mafunzo pepe ya Kiarabu katika kiwango cha kieneo na kimataifa.

# Arabic-Online.net
# العربية على الإنترنت

**Maono:** Kusambaza Kiarabu duniani.

**Mission:** Kutoa elimu bora kwa wanenaji wasio wa asili ya Kiarabu, kufikia viwango vipya vya kimataifa na maadili mema katika kujifunza na kufunza lugha, kupitia njia anzilishi ya mtandaoni ambayo husaidia kusambaza lugha na utamaduni wa Kiarabu duniani kote.

Mpango huu ni ufanisi muhimu na njia mpya katika historia ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili, na kwa hakika itaongoza mtazamo mpya wa kufahamu utamaduni.

Arabic-Online.net itawaruhusu wanenaji wasio wa asili wa Kiarabu kujifunza lugha hii ya dunia. Itawapa pia wanenaji wa Kiarabu walio ng'ambo na watoto wao, wanaoishi katika mazingira yasio ya Kiarabu ambayo yanaonekana yana upungufu wa ujuzi wa kimsamiati na kusoma na kuandika, nafasi ya kushughulikia upungufu huu.

Arabic-Online.net itafikia mahitaji ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili kwa kutoa mpango uliojumuishwa usio wa kawaida mtandaoni ambao huruhusu mafunzo ya Kiarabu mahali popote duniani, yasiyozuiwa na muda au nafasi, na hata pia vizuizi vya usafiri na mwenendo.

# Malengo ya Arabic-Online.net

1. Kufikia mahitaji ya nyanja ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili kwa kutoa mpango tondoti na uliojumuishwa wa mtandaoni, kufikia mtalaa mahiri wa kielimu wenye mitihani iliyosawazishwa kwa njia ya juu zaidi ya mafunzo ya lugha.
2. Kufikia hitaji linaloongezeka kutoka kwa wanenaji wa lugha nyingine la kujifunza lugha ya Kiarabu.
3. Kuchangia usambazaji wa lugha ya Kiarabu, kuboresha jukumu lake, kukuza hali yake ya juu kama lugha kuu, na kuimarisha jukumu la Saudia katika kutoa Kiarabu.
4. Kuchangia usambazaji wa utamaduni wa Kiarabu na Kiislamu, kuhusika kabisa katika kukuza ufahamu wa pamoja na kuishi kwa amani kati ya tamaduni mbalimbali, na kufikia mahitaji ya mawasiliano ya utamaduni kati ya wanenaji wa Kiarabu na watu wengine duniani.
5. Kutoa Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili katika kiwango chake cha saa na umbo lake la matumizi, kwa kulenga matumizi ya kila siku.
6. Kusaidia kukuza nyanja ya kufunza Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili kwa kuwasilisha maudhui ya mtandaoni ambayo yanafikia viwango wa dunia.
7. Kuwasilisha mafunzo pepe yaliyojumuishwa, ingiliani ya Kiarabu kwa wanenaji wa lugha nyingine.

**796**
videokuu ingiliani

**6,320**
picha



**12,000**
faili za sauti

**10,076**
mazoezi


## Viwango vya Kufunza

Viwango vya kufunza vya mpango huu hutegemea Mpangilio wa Kawaida wa Ulaya wa Kurejelea Lugha. Kwa hivyo kozi hii huleta, katika umbo lililojumuishwa, ujuzi ain nne wa lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika), na vijenzi vikuu vya lugha (sauti, msamiati na muundo). Mpango huu huzingatia ubora wa kiisimu, mawasiliano na utamaduni kwa wanafunzi kwa kuwapa polepole nyenzo kulingana na viwango vya ubora wa wanafunzi. Mpango huu hujumuisha muundo wa mtandaoni na wa kujifunza mwenyewe, kutumia jukwaa kuu la kujifunza lugha lililotengenezwa na Rosetta Stone.

Mahali pa kuanzia pa Arabic-Online.net ni mtihani wa ufahamu, ambapo wanafunzi watabainisha kiwango cha darasa watakachochukua. Mpango kwa kawaida huanza na kijenzi fonemu cha ufahamu. Awamu hii huonyesha sauti za Kiarabu (ubunifu kamili wa sauti za Kiarabu na hali ya kujieleza hutolewa), herufi za Kiarabu na tofauti mbalimbali za grafemiki. Mpango huu una viwango 16, na mitihani ya ufanisi hupangwa mwisho wa kila awamu 6.

Wanafunzi wanaokamilisha mahitaji ya mpango hupewa cheti cha ustadi wa Kiarabu kwa wanenaji wasio wa kiasili na kuidhinishwa na Chup kikuu cha Mtandaoni cha Saudia.

# Viwango vya Mpango



## Saa za Kufunza

4Viwango tofauti hugawanywa kwa modyuli 96 zenye masomo 416, na kila kiwango kinajumuisha masomo 24. Kati ya idadi jumla za masomo, masomo 28 hushughulikia ufahamu fonemiki. Mpango wote hushughulikiwa kwa saa 980, 60 kwa kila kiwango (saa 48 kujifunza mwenyewe, saa 12 vya mwonyesho pepe). Mpango una asimilia 75 wa kujifunza mwenyewe na madarasa ya mtandaoni ya asilimia 25

## Vijenzi vya masomo

Kila kiwango kina modyuli 6 (vizio), kila moja kina masomo 24, pamoja na video kuu, misamiati, miundo, kusoma, mazungumzo, kuandika na hata pita mazoezi mbalimbali (video 796, faili za muziki 12000, picha 6320, mazoezi 10076).


60
saa 60 kwa kila kiwango
48
saa 48 (kusoma mwenyewe) kwa kila mwezi
12
saa 12 za mtandaoni kwa kila kiwango kila mwezi
15
saa 15 kila wiki
12
saa 12 za kusoma mwenyewe kila saa kila wiki
3
saa 3 za mtandaoni kila wiki
20
Vijenzi 20 wa Ufahamu Fonemiki
15
saa 15 za kusoma mwenyewe za Fonemiki
5
saa 5 za Fonemiki
saa 980 kwa kila kiwango
25% za madarasa ya mtandaoni
75% za kusoma mwenyewe


Vizio na Masomo
96
Vizio 96 vya elimu (modyuli)
412
Masomo 412 katika viwango vyote
6
saa 6 kwa kila kiwango
24
Masomo 24 kwa kila kiwango
4
Masomo 4 kwa kila kizio
28
Masomo 28 ya ufahamu fonemiki


Vijenzi vya masomo
Video kuu ya kusikiliza
Miundo
Msamiati
Kuandika
Mazoezi
Mazungumzo
Kusoma

## Nafasi za ajira

Arabic-Online.net, inayotegemea madarasa ya mtandaoni, inatarajiwa kutoa zaidi ya nafasi 10,000 za ajira kwa walimu wa kiume na kike, ambayo itaimarisha mojawapo ya malengo ya Wizara ya Elimu ya Saudia na Chuo kikuu cha Mtandaoni cha Saudia, kwa jina kutoa nafasi za kazi za masomo ya mbali.

Kwa hivyo Arabic-Online.net sio mpango tu wa elimu; ni maono na mwito unaojumuisha kila kitu

.


Arabic-Online.net
العربية على الإنترنت
About the Program
Program Levels
Units and classes
Lesson components
Studying Hours
Registration
Latest News
FAQ
Vacancies
LEARN THE ARABIC LANGUAGE USING THE LATEST INTERACTIVE TECHNOLOGIES


Arabic-Online.net
العربية على الإنترنت





## Mawasiliano:

Kingdom of Saudi Arabia- Riyadh- Abu baker road.
P.O Box 93499 Zip code: 11673

Nambari ya simu: 0996112613500 ext. 3321

Barua Pepe: ArabicOnline@SEU.EDU.SA



Arabic Online

العربية على الإنترنت

Arabic-Online.net